

KONGAMANO PAMOJA NA MUNGU



Bila shaka kabisa ni majaliwa kwangu kuwa hapa usiku wa leo, huku chini kabisa Tifton, Georgia. Lakini sikujua kabisa kwamba nilikuwa ninaenda kuwa na majaliwa ya kuja hapa kwenye kanisa hili, lakini tuna furaha kuwa hapa. Ndio kwanza ningie dakika chache zilizopita, nasi tunaona ya kwamba hiki chumba, ama nje na ndani kwa namna fulani kimejaa kidogo.

² Kwa hiyo, usiku wa leo tulifikiri tu tungekuwa na wakati kidogo wa kufahamiana ili kuelewana vizuri, kwa sababu tuna siku mbili zaidi za ibada zinazokuja. Nilikuwa na mara yangu ya kwanza, nadhani, kadiri nijuavyo kupeana mikono na Ndugu Perry, mchungaji. Nasi tunakuja kwa mwaliko wa rafiki yetu mpendwa na ndugu, Ndugu Evans.

³ Nasi tulikuwa na muda kidogo wa kupumzika wakati tukishuka kuja wakati huu, tunajiandaa kuondoka sasa kwenda ng'ambo kwa ajili ya sehemu kubwa ya ulimwengu katika miezi michache ijayo. Sisi, mara baada ya haya tunaenda kwenye Visiwa vya Karibea, na kutoka huko tuingie Afrika Kusini, turudi Uswisi, Uholanzi, Uingereza, hadi Norwe, turudi, tuingie Australia, Sydney na Melbourne, juu turudi India, kupitia njia hiyo, tukirudi kupitia nchi takatifu, Bwana akipenda, mwaka huu ujao. Kwa hiyo, tulikuwa na wakati ambapo tungeweza tu kuzunguka na kuwatembelea, labda, watu ambao hatukuwa tumekutana nao, bado.

⁴ Naye Ndugu Welch Evans, akiwa ni ndugu wa thamani sana, naye alikuwa ameniomba mara kadhaa nishuke nje huku. Nami nilikuwa huku chini si muda mrefu uliopita, kumtembelea nyumbani kwake, ndipo nikajaribu kuvua samaki wawili watatu huku, lakini sijui nilifanikiwa vizuri vipi, sidhani vizuri sana. Lakini nilitaka kurudi kukutana na Wakristo. Nami nilifikiri hii ingekuwa ni nafasi nzuri ya kutumia siku hizi mbili tatu huku chini pamoja nanyi watu.

⁵ Mara nyingi, huduma yangu ni kuwaombea wagonjwa. Mimi...Hapana shaka ila kwamba, kupitia magazeti, na majarida, na kadhalika, kwamba mmesikia habari za wema wa Bwana Yesu, jinsi ambavyo ame—amewaponya wagonjwa na kufanya maajabu makubwa na ishara.

⁶ Tukija usiku wa leo, tumeona ingekuwa karibu haiwezekani kabisa kupanga mstari wa maombi, kuna wengi walio kote nje, kama walivyo ndani. Kesho watachukua jumba la mikutano,

ama wanajaribu kulipata, ile shule ya upili, ama chochote kile, watawaambia habari zake, nafikiri wanakusanyika juu yake sasa, ambamo tunaweza kupanga mstari, ili tuweze kufanyiza mistari ya maombi na kuwaombea wagonjwa ibada zijazo, kuanzia kesho usiku. Popote ibada zitakapokuwa, tutajaribu kukimbia kule na kugawa kadi za maombi na kuwapanga watu mistarini kusudi muweze kuja kwa namba, kwa kuwa imekuwa ndio mfumo katika ibada zetu, sikuzote, kufanya hivyo.

⁷ Kwa hiyo, hilo litatangazwa kesho, labda. Nao watakuwa na ubao hapa nje kama upo, mahali tu ambapo ibada, kwamba itakuwa kwenye ukumbi gani, kesho usiku. Na—na kama mkija huku, watakuwa na ubao uliowekwa pale nje. Kama itatubidi kuendelea hapa, mbona, njoni moja kwa moja karibu saa kumi na mbili, na, ama saa moja, ama wakati wowote ule, saa kumi na mbili u nusu, saa moja, nasi tutagawa kadi. Na basi kama itatubidi kurudi nyuma na kuanza upya tena, mbona, tuta—tutawapanga watu mstarini ambapo tunaweza kuwaombea. Hivi, ingekuwa vigumu sana. Lakini tutafanikiwa kwa njia fulani.

⁸ Sasa, ni wahudumu wangapi walio hapa ndani? Ningeweza kuona, kuwaona tu mkiinua mikono yenu? Hilo ni zuri sana. Vema, salamu kwenu, rafiki zangu wa thamani katika Kristo.

⁹ Sasa, katika kuzungumza juu ya . . . Hiyo ni, kuhusu mhubiri mdogo kiumri kuliko wote niliopata kuona, yeye ni mmoja hapa mwenye umri wa kama miaka miwili, aliinua mkono wake. Mimi—mimi, huyo, nilifikiri Maskini David Walker karibu ndiye aliye mdogo kuliko wote niliyepata kumwona, lakini huyu amemshinda. Vema, huyo ni mwana mzuri sana. Nina mmoja nyumbani kama huyo, anayedai atakuwa mhubiri, lakini kama akiwa mhubiri, itambidi kujirekebisha sana.

¹⁰ Alikuwa mbaya sana hivi majuzi. Alifanya kituko, akawaweka maskini dada wote wawili kwenye kiti. Ninyi akina baba na mama mnajua ninalomaanisha. Nikasema, “Mwanangu, uliendelea kuniahidi kwa muda mrefu, utakuwa mzuri. Utakuwa mwema lini?”

¹¹ Akasema, “Nitakapokuwa mhubiri.”

¹² Mama yake akasema, “Itakubidi kuushinda huo, la sivyo hutakuwa mhubiri.” Wanaweza kuuchochea moyo wako katika mambo yao madogo madogo ya mzaha wanayosema.

¹³ Sasa usiku wa leo, huko nje kuna baridi, kwangu mimi, nilifikiri nilikuwa nikishuka kuja huku niende miguu mitupu tena, lakini ningeninii, naona ningeganda kama ningefanya hivyo. Kwa hiyo, wengi wamesimama nje, kote kwenye majengo, na kadhalika. Wengi, wengine huko nje kwenye magari yao na magari yangali yanaingia. Kwa hiyo hatutawaweka muda mrefu, ni kuwazungumzia tu na kujaribu kuinua imani kwenu ili tutakapofikia kuwaombea wagonjwa, ili mweze kupokea.

¹⁴ Nafikiri ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni jambo ambalo unapaswa kuliendea kwa uchaji, kwa akili timamu, kwa sababu ni kazi ya Mungu. Sasa, Mungu kamwe hawezi kwenda kinyume na sheria na kanuni Zake Mwenyewe, daima atafanya kazi kulingana na kanuni Zake.

¹⁵ Ni kama tu ikiwa wewe, nimesema jambo hili mara nyingi, kama ulikuwa na kilima *hapa* na kisima kikubwa cha chemchemi, kikirusha tu maji hewani, nawe ulikuwa na kilima kingine *hapa*, nacho kilikuwa kimetoa mazao nayo hayo mazao yalikuwa yanakauka yakihitaji maji, sasa ungeweza kusimama juu ya kilima hiki na kuyapigia yale maji makelele, “Njoni huku, njoni huku mkayamwagilie maji haya mazao!” Kamwe hayatafanya hivyo, la hashu, kamwe hayatafanya hivyo. Lakini kama utafanya kazi kulingana na kanuni za uvutano, unaweza kuyapitisha maji hayo moja kwa moja kilimani, na kuimwagilia mimea yako. Lakini huna budi kutumia kanuni fulani kufanya hivyo, nayo itafanya kazi kikamilifu kila wakati.

¹⁶ Kama ungali kuwa hapa nje uwandani usiku wa leo, na kuna giza jinsi kulivyo, nawe ungesema, “Mimi ni mwanasayansi, nami ninajua ya kwamba kuna umeme wa kutosha katika hewa hii kuangazia uwanja huu, na kunionyesha jinsi ya kutoka hapa. Loo, ewe umeme mkuu, najua uko hapa. Utafiti wa kisayansi unaonyesha ya kwamba uko mumu humu hewani. Tenganisha hewa baridi na moto kwa, na kuileta pamoja, unao umeme. Na sasa, niangazie tu njia kwa sababu nimepotea.” Ungeweza kupiga mayowe mpaka ukapwelewa na sauti, wala kamwe hakungewaka, lakini kama ukifanya kazi kulingana na kanuni za umeme, utaangaza njia. Unaona?

¹⁷ Sasa hivyo ndivyo ilivyo kuhusu Mungu. Uponyaji wa Kiungu umetumiwa vibaya mara nyingi, unaona, lakini kuna njia. Upo, kweli, uponyaji wa Kiungu, bali hatuna budi kutenda kazi kulingana na kanuni na amri za Mungu kuufikia uponyaji wa Kiungu. Upo.

¹⁸ Wakati mwingine unashangaa ni kwa nini wengine wanaponywa, na wengine hawaponywi. Vema, ni kwa sababu mmoja anaweza kuja kwa njia ya kanuni, na huyo mwingine anajaribu kupitia njia ya mkato. Ila Mungu hana njia za mkato, sote tunapitia njia ile ile. Hakuna upendeleo kwa Mungu.

¹⁹ Kwa hiyo usiku wa leo, nilifikiri ngingezungumza tu nanyi kwa namna fulani nipate kufahamiana nanyi. Nami ni mgeni kwenu, nanyi ni wageni kwangu, lakini hata hivyo, sisi si wageni, sisi ni ndugu wa thamani, dada wa imani iliyo katika Kristo Yesu. Sisi ni wasafiri hapa na wageni, sisi ni wageni pamoja, tukiutazamia Mji, ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu, huko ndiko tunakotamani kuwa, nasi tunasafiri pamoja huko.

²⁰ Sasa, kabla sijasoma sehemu ndogo tu ya Maandiko hapa, kifungu kimoja, ama *kitu kingine*, hebu na tuinamishe vichwa

vyetu kwa muda kidogo tu, ndani na nje, mkipenda, watu wa thamani, huku tukizungumza na Bwana wetu wa thamani.

²¹ Baba yetu wa Mbinguni Mwenye Neema, kweli ni majaliwa makuu tuliyo nayo usiku wa leo, kuja na kukuita Wewe Baba yetu. Tukijua ya kwamba tumepita toka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu:

*...Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa
Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee,
bali awe na uzima wa Milele.*

²² Nasi tuna furaha sana, Bwana, usiku wa leo, ya kwamba sisi ni washiriki wa neema Yake na wa Uzima huu wa Milele. Hakuna kitu ambacho tumefanya, wala hakuna chochote ambacho tungeweza kufanya, ambacho kingestahili baraka kama hizo, bali ni kwa neema kuu ya Mungu. Nasi tunaikubali kwa unyenyekevu na kuiamini, na tunawaambia wengine kwa shauku juu ya Njia ya Mungu, Njia iliyoandaliwa ya kuiepuka ghadhabu ya Mungu kwenye Siku ya Hukumu, na kuwa rafiki Yake, kuingia katika Uwepo Wake pamoja na nafsi zilizoosha kwa Damu ya Mwanawe, Kristo Yesu.

²³ Pia tunafundishwa na Neno Lako lenye neema sana, Bwana, ya kwamba "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Loo, usiku wa leo tunapowazia jambo hilo, wakati Daudi alipopaza sauti na kusema:

*Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA: vyote vilivyo ndani
yangu vilihimidi jina lake takatifu.*

*Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, wala usizisau
fadhili Zake zote:*

*Akusameheaye maovu yako yote; na akuponya
magonjwa yako yote;*

²⁴ Jinsi tulivyo na furaha usiku wa leo, Bwana, kujua kwa hakikisho hili lililobarikiwa tulilo nalo, kwamba kuna mgawo wa faida unaoweza kupatikana kwa hati ya mkataba!

²⁵ Nasi tunaomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba Wewe utatubariki kwa njia ya kipekee. Ninapoangalia, wakisimama nje ya madirisha wanaposhuka kuja kwa milolongo ya—ya magari, na kuona hiyo mioyo ya thamani, yenye njaa, wamesimama huko nje huku wameinamisha vichwa vyao na kungojea baraka kutoka kwa Mungu, au kusikia kitu ambacho kingewazungumzia amani, au kingewatia moyo safarini, tunaomba ya kwamba Wewe uwabariki, wale wanaosimama kote sakafuni, na kuzunguka kuta na marefu, wameketi, wengine kwenye magari. Ee Bwana, jalia kusiwe na nafsi yenye njaa inayoondoka bila kushibishwa kila shauku wanayokuja nayo. Wajalie, Bwana.

²⁶ Kama kuna yeyote katika Uwepo wa Kiungu ambaye ni mgonjwa na mhitaji, naomba watoke kwenye mkutano huu usiku

wa leo, wazima. Kama kuna yeyote asiye na tumaini, bila Mungu, bila Kristo, jalia waende wakiwa na kikombe kinachofurika kwa furaha, kwamba wamempata Yesu, Chemchemi isiyokauka ya Uzima wa Milele. Tujalie, Bwana. Yasikie maombi yetu, na useme nasi kupitia Neno Lako. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁷ Katika Ki—Kitabu cha Isaya, ningependa kusoma, kwa muda kidogo tu, sehemu ya Maandiko, nitachukua mlango wa kwanza na kifungu cha 18. Sote tunakijua, lakini ningetaka tu kukisoma.

Haya, njoni... tusemezane, asema BWANA: dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa... nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.

²⁸ Ni fungu la kale la Maandiko linalojulikana sana. Nami nililiwazia tu wakati nikishuka kuja leo hii, nami nilikuwa nikiwazia hilo ni jambo la kushangaza, wakati Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, angealika kiumbe Chake, wanadamu, kuja kuhojiana Naye. Ni heshima jinsi gani kwa Mungu kutoa mwaliko!

²⁹ Mnajua, haikumbidi kufanya hivyo, bali alifanya hivyo. Naye akamwalika “yeyote atakaye, na aje.” Yeye hakumchagua tu mtu fulani, ama kundi fulani, au dhehebu fulani, ama rangi fulani, alisema, “Atakaye, na aje.” Na basi nina hakika ya kwamba hiyo inamaanisha kila mmoja wetu ana haki.

³⁰ Hilo linanifanyia vizuri zaidi usiku wa leo, kujua jambo hilo, kuliko ingalikuwa kama Maandiko yangesema, “Hebu William Branham aje,” kwa sababu huenda kukawa na zaidi ya William Branham mmoja. Lakini aliposema, “yeyote atakaye,” ninajua ya kwamba inanijumuisha mimi, na inakujumuisha wewe, nasi sote tuna haki kwa Mti wa Uzima.

³¹ Kuna mambo mengi ambayo tungeweza kuheshimiwa kwayo: Mhudumu fulani anaweza kutualika kwenye kanisa fulani, na ingekuwa ni heshima; jamii fulani ya mjini huenda ikatualika makazini mwao, na ingekuwa ni heshima; ama ningesema hivi: Vipi kama rais wetu mpendwa, Dwight Eisenhower, alimwalika Mwanademokrati aliye bora kuliko wote aliyeko Tifton, aje amtembelee? Ingawa alitofautiana naye katika siasa, ingekuwa ni heshima kwake, kwa sababu Rais Eisenhower anaita.

³² Nami ningesema hivi: Kama angefanya jambo kama hilo, tungejivunia hilo kote nchini, kwamba Rais Eisenhower alitualika kuja Ikulu kuzungumzia mambo pamoja naye. Mbona, magazeti yangelitangaza, radio ingejaa hilo, televisheni ingelitangaza kila mahali, kwa sababu kwamba Rais Eisenhower alitualika kuja kwenye Ikulu kulizungumzia pamoja naye. Ni heshima iliyoje! Hakika tusingeukataa.

³³ Lakini wazia, kwamba Mungu alitualika! Mungu wa Mbinguni alitualika mimi na wewe, maskini watu wenye kikomo, maskini, na kutualika tuje Kwake na kulizungumzia kuhusu Uzima wa Milele, “dhambi zetu zikapokuwa nyekundu sana, hata hivyo zitakuwa nyeupe kama theluji.” Ni zaidi ya chochote ambacho ningeweza kuwazia, kwamba Mungu anajaribu kuhojiana na viumbe aliowaumba. Lakini Yeye alitualika tuje.

³⁴ Naye hakika amekataliwa na watu wengi. Na kama tukiukataa mwaliko kama huo, basi tusingeweza kutarajia kubarikiwa wakati wa kuja Kwake kwenye Hukumu.

³⁵ Kwa maneno mengine, Mungu anasema jambo kama hili: “Njoo na tuketi chini tulizungumzie.” Ninapenda chochote kama hicho.

³⁶ Wakati fulani uliopita huko Phoenix, Arizona, kulikuwako na wasichana kadhaa wa Kihindi waliokuja mkutanoni, nao wakaimba wimbo kwenye uwanja wa michezo huko nje, na kusema, “Ningependa kulizungumzia pamoja na Yesu, na kumwambia rehema Zake zote.” Nami nikawazia juu ya wimbo huo, na juu ya Maandiko haya. *Ningependa Kulizungumzia Pamoja Naye.*

³⁷ Inanikumbusha juu ya m—mzee mmoja mweusi, wakati mmoja, alikuwa akiimba wimbo, na kabla tu hajamaliza, ama, kuanza kuimba, akasema, “Mnajua,” akasema, “nimemwambia Bwana muda mrefu uliopita, ya kwamba wakati wangu wa kuondoka ufikapo, kwamba sikutaka shida yoyote kule chini mtoni. Kama kuna jambo lolote baya, hebu tulizungumzie sasa.”

³⁸ Nami nafikiri huo ni usemi mzuri tu kama ule ningeweza kupata, “Sitaki shida yoyote mtoni.” Itakuwa asubuhi yenye huzuni. Wakati Meli hiyo itakapoondoka, ninataka kuwa na tiketi yangu mkononi mwangu, na kujua ya kwamba imelipiwa, kujua ya kwamba kila kitu ni sawa, maana, hakutakuwa na wakati wa kulizungumzia wakati huo, afadhali tulizungumzie sasa.

³⁹ Mungu alisema, “Hebu na tusemezane jambo hili.” Tusemezane, kama wewe ni mgonjwa, hebu na tusemezane na Mungu. Kama daktari alisema ya kwamba huwezi kupona, basi hebu na tukipeleke kisa hicho kwa Mungu, tuketi chini na kusemezana Naye, “Bwana, nimefanya kosa, lakini kama utanijalia tu nipone, nitakutumikia Wewe maishani mwangu mwote.” Lizungumzie tu pamoja Naye. Nafikiri lingekuwa ni jambo zuri kwetu kufanya hivyo kabla ya ibada kesho usiku, tuwe na “kulizungumzia” kidogo na Kristo.

⁴⁰ Kwa maneno mengine, Mungu anasema, “Njoni tufanye kongamano pamoja, tukutane katika kongamano, ndipo tulizungumzie.”

41 Kwa kawaida, tunasikia mengi sana hivi karibuni, kuhusu makongamano kufanywa kila mahali. Na kongamano ni nini?

42 Tulisikia hapa, wakati fulani uliopita, wengi wenu ninyi watu wa rika yangu, mnakumbuka katika Vita vya I vya Dunia, walikuwa na kile kilichoitwa Kongamano la Mabingwa Wanne, ambapo Mabingwa Wanne wa nchi huru ulimwenguni walikutana pamoja katika kongamano. Ndipo wakafanya Kongamano la Geneva; walikuwa na Kongamano la Paris. Bw. Eisenhower ndiyo kwanza aende kwenye ulimwengu huru, akifanya makongamano.

43 Na Mungu anaagiza kongamano. Mambo haya yote makuu na tajiri katika Neno la Mungu, yanatufanya sisi watu matajiri kujua kwamba Mungu ametupa mwaliko wa kuja kuzungumza na Yeye kabla ya wakati.

44 Siku moja, kulikuwa na mwanamke maskini hohehahe, hapa mijini. Na hali yake ya kifedha ilikuwa duni sana, hata ilikuwa inaenda kuwalazimu kuleta watu wa jimbo kumsaidia. Ndipo wachunguzi walipokuja na kumwambia mwanamke huyu, “Imekuwaje kwamba wewe ni maskini sana hata inakubidi kuomba jimbo likusaidie?”

45 Naye akatoa hadithi ya mume wake kuwa amekufa, na kumwacha na mwana mmoja, naye mwana huyu akawa mfanyabiashara, naye alikuwa amehamia India. Naye hakuwa amepokea hata senti moja kutoka kwake kwa miaka *kadha*, lakini alikuwa amepokea baadhi ya barua tamu sana alizowahi kusoma. Kisha kasema, “Labda yuko katika hali mbaya sana hata asingeweza kunisaidia. Naye ni mvulana mzuri sana,” kasema, “Si—sitaki kumwomba chochote.”

Kisha kasema, “Unamaanisha kwamba mwanao, mfanyabiashara, amekutumia tu barua, na hizo tu ndizo alizotuma?”

46 Ndipo yule mama mzee mbarikiwa akatoa maskini miwani yake, na kuiweka juu ya pua yake, na kusema, “La, alinitumia baadhi ya picha nzuri sana nilizopata kuona.” Naye anaingia kwenye Biblia yake na anatafuta-tafuta kwenye Biblia yake kwa muda kidogo, kisha anachukua furushi kubwa mno la vipande vidogo vya karatasi, na kuvitandaza kwa hao wapelelezi. Kasema, “Angalieni tu ni picha za kupendeza jinsi gani!”

47 Basi wakati mpelelezi alipokwisha kuzisoma, zilikuwa ni hati za benki. Alimiliki maelfu ya dola, wala hakuja hilo.

48 Hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo, kwa watu wengi, kama tungepitisha tu vidole vyetu kwenye Biblia ya ahadi za Mungu, sisi ni zaidi ya mamilionea wa utajiri wa neema Yake. Ingawa, haidhuru tulikuwa tumefanya nini, “Njoni, tusemezane,” asema Mungu.

49 Yeye ametupa ahadi, bali tunafikiri tu Biblia ni kitu ambacho wahubiri pekee wanapaswa kusoma, ama kwamba watu fulani wana ma—mahojiano yake yote. Ni kwa yeyote atakaye. Kila ahadi ni nzuri tu leo hii, kama ilivyokuwa siku ilipoandikwa katika Biblia.

50 Mungu akiwaita watu Wake kwa makongamano. Kongamano ni la nini? Kwa nini linatukia? Ni wakati dharura inapotokea. Hapo ndipo mataifa yanapokusanyika yaliyo na msimamo mmoja, wanaamini katika jambo fulani na wanakutana kwa mapatano na makubaliano ya pamoja. Kisha wanachagua mahali fulani pa kufanya kongamano hili. Kwa kawaida mahali ambapo ni pazuri na mahali ambapo wanaweza kujisikia wamestarehe pamoja, kwa sababu hawana budi kuwa katika ubora wao wapate kufanya mapatano yao. Ndipo, mapatano yao yatakapofanywa, basi wao, vema, jambo wanalofanya basi, baada ya mapatano haya kufanywa, wanaanza kuyafanya kazi.

51 Na hivyo ndivyo Mungu anavyofanya makongamano Yake. Hebu turudi nyuma na tuwazie juu ya makongamano machache ambayo Mungu amefanya kabla ya hili usiku wa leo. Kongamano la kwanza ninalotaka kulizungumzia sasa hivi kwa muda mfupi, tungeliita Kongamano la Edeni.

52 Neno lilikuwa limefika tu Mbinguni kwamba mtoto wa Mungu alikuwa ameanguka kutoka kwa neema, alikuwa ametenda dhambi, ndipo hali ya hatari ikatangazwa. Ilibidi Mungu kuwaleta Malaika na waje kutoka Mbinguni, kwa sababu mtoto Wake Mwenyewe alikuwa ameanguka na kuziasi amri Zake. Na ilikuwa ni adhabu ya kifo kwa kutotii amri hizi. Ilibidi Mungu aje katika hali ya hatari, kama vile kongamano lolote linavyofanywa.

53 Lazima jambo fulani lifanywe, la sivyo yote yatakuwa ni machafuko, uumbaji Wake Mwenyewe. Ndipo Mungu akachagua mti fulani, na akawaita Adamu na Hawa pamoja na kuwaleta na kufanya kongamano pamoja nao. Ndipo alipofikia uamuzi, alifanya njia ya kuepukia kwa ajili ya wanadamu Wake. Naye akasema, “Uzao wako utakiponda kichwa cha nyoka, na kichwa chake kitaponda kisigino chako.”

54 Pia kulikuwa na wakati mwingine ninaoweza kukumbuka, wa kongamano lililoitishwa na Mungu, nasi tungeliita hili Kongamano la Kichaka Kinachowaka Moto. Mungu alikuwa amekumbuka ya kwamba alifanya ahadi kwa Ibrahimu, na kwa, si kwa Ibrahimu tu, bali kwa Uzao wake baada yake. Nasi ni Uzao wa Ibrahimu. “Tukiwa wafu katika Kristo, tunachukua Uzao wa Ibrahimu na ni warithi sawasawa na ahadi.” Mungu alikumbuka ya kwamba alifanya ahadi, kwamba hao wazao wangekaa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne, bali Yeye angewakomboa.

⁵⁵ Naye nabii ambaye Yeye alikuwa amemchagua na kumzaa nabii ulimwenguni, yeye, badala ya kupitia njia ya Mungu, aliendea njia ya kiakili. Alikuwa ameshuka kwenda Misri na alikuwa ameelimishwa, na alikuwa na e—elimu kubwa, akajifunza kila namna ya mbinu za kijeshi, kisha akajaribu kuiteka kwa njia yake mwenyewe ya kuifanya.

⁵⁶ Kuna njia mbili tu za kufanya jambo lolote, na hiyo ni njia sahihi, na njia mbaya; na hiyo ni njia yetu, na njia ya Mungu. Njia yetu kila mara, daima ni mbaya; njia za Mungu daima ni sahihi. Haidhuru inaonekana ya kijinga jinsi gani kwetu, jinsi ilivyo rahisi, Mungu nyuma yake, hakuna kitu kinachoweza kuizuia. Mungu hulisema katika amri Zake, na njia Zake zinafanya kazi kikamilifu.

⁵⁷ Kwa hiyo, tunaona Mungu akimwita Musa, ama, kumwona Musa, nabii mtoro. Musa akawazia, hakika, ya kwamba alikuwa na nguvu za kutosha na alikuwa na nia ya kijeshi vya kutosha, kuwakomboa wana wa Israeli.

⁵⁸ Sasa ninawatakeni mpate jambo fulani hapa: Mungu, alipomwumba mwanadamu, alimpa hisi tano. Na hizo hisi tano ni kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia, kama sote tujuavyo. Hisi hizo tano hazikupewa mtu kumwongoza, hizo alipewa mtu kuwasiliana na makazi yake ya duniani, kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Na hizo ni hisi zako za duniani, wala hukupewa zikakuongoze, bali Mungu alimtuma Roho Mtakatifu, Naye ndiye Kiongozi wako, ile hisi ya sita, inayokufanya uamini mambo ambayo huwezi kuona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kusikia.

⁵⁹ Hiyo hisi ya sita, kitu kinachokuinua, na ni tabaka moja tu la watu lililo na hiyo hisi ya sita, hao ni waaminio. Waebrania 11:1 ilisema, “Kwa imani! Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu.” Kwa hiyo, Mungu humpa mwanadamu imani. Nayo imani ndiyo hisi ya sita inayokufanya ukane chochote ambacho ni kinyume na Neno Lake.

⁶⁰ Alimpa Musa imani hiyo alipokuwa, hisi hiyo ya sita, alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye Sara sitini na mitano. Tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa, alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na saba, bila watoto. Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, sawa na aliyekufa, naye Mungu akamwambia atapata mtoto. Naye aliita chochote kinyume chake, kana kwamba hakikuwa, kwa kuwa alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba Mungu aliweza kutimiza kila Neno alilosema.

⁶¹ Hakungojea tu kutoka usiku mmoja hadi mwingine, alingojea miaka ishirini na mitano kabla halijatukia, bali hakushindwa hata wakati mmoja. “Hakusita katika ile ahadi kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu.” Alikuwa na mguso wa hisi hiyo ya sita, aliita chochote kinyume

na kile Mungu alichosema, kana kwamba hakikuwa. Yale Mungu aliyosema yalikuwa ni kweli, na baada ya miaka ishirini na mitano mtoto huyo akazaliwa.

⁶² Loo, najua linaonekana la kijinga kwa akili ya mwanadamu. Ungeweza kuwazia mzee mmoja hapa Tifton, mwenye umri wa miaka mia moja, na mwanamke tisini, wakishuka kwenda kwa daktari kufanya maandalizi ya kupata mtoto? Mbona, daktari angesema, “Huyo mzee kidogo ameguswa kichwani mwake, kuna kasoro.” Hiyo ni kweli. Katika kisa cha Ibrahimu, alikuwa ameliamini Neno la Mungu, na daima ni kichaa kwa nia ya kimwili.

⁶³ Vema, hiyo ni hazina ya thamani katika nia ya Mungu, na katika moyo wa Mungu, kwamba Yeye anaweza kumtumia mtu huyo. Mpaka tutakapofikia mahali ambapo ha—hatuzitegemei hisi hizi tano, za kuwasiliana na makazi ya duniani, na kutembea kwa imani, “Kwa kuwa mwenye haki ataishi kwa imani.”

⁶⁴ Musa alihitaji mguso huo, alijaribu kufanya hivyo kiakili. Hiyo ndiyo shida ya makanisa ya siku zetu, tunajaribu kufanya hivyo kupitia shule, tunajaribu kufanya hivyo kupitia madhehebu, tunajaribu kufanya hivyo kupitia elimu, na matengenezo. Kile kanisa linachohitaji ni ku—kuzaliwa upya, ubatizo wa Roho Mtakatifu, mguso wa hisi ya sita ambao huiwasha nafsi moto kwa ajili ya Mungu, mguso huo wa kumtoa kwenye uozo huo.

⁶⁵ Wanapoanza kusema, “Siku za miujiza zimepita, na hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu,” Mungu anahitaji kuligusa kanisa hilo, kuagiza kongamano. Kwa nini tutilie shaka Neno Lake?

⁶⁶ Kwa hiyo akaagiza kongamano pamoja na Musa, Naye akachagua mahali, kichaka kinachowaka moto. Na kwenye kichaka hicho kinachowaka moto, Yeye akazungumza na Musa na kusema, “Ninakumbuka ahadi Yangu, nami ninakutuma huko chini, ambako ulishindwa, bali ninakurudisha moja kwa moja ukachukulie mahali ulipoachia, lakini wakati huu, itakuwa ni tofauti.” Musa, mwoga, akimkimbia Mungu.

⁶⁷ Loo, wakati mwingine unapowasiliana na Mungu na kufanya kongamano pamoja Naye, Naye anakugusa, na kuishusha hiyo hisi ya sita, nguvu hizo, inakufanya ufanye mambo ambayo watu wanafikiri wewe una kichaa.

⁶⁸ Angalieni ni tofauti jinsi gani: Mwoga akikimbia nyuma ya vichaka kuwachunga kondoo wa Yethro siku moja, alikutana na Mungu katika kongamano kwenye kichaka kinachowaka moto, na kesho yake, huyu hapa anashuka kwenda Misri, mzee, mwenye umri wa miaka themanini, nywele nyeupe na ndevu zikining’inia usoni mwake, mkewe ametagaa juu ya nyumbu akiwa na mtoto nyongani mwake, fimbo mkononi mwake, ndevu nyeupe, akienda.

“Kwani unaenda wapi Musa?”

⁶⁹ “Ninashuka kwenda Misri kuiteka.” Uvamizi wa mtu mmoja, lakini jambo ni kwamba, aliiteka, kwa sababu alikuwa amefanya kongamano na Mungu. Naye akaguswa na kitu kilichokuwako, akabadilisha nia yake. Akasahau theolojia yake, na kuamini Neno la Mungu. Kasema, “Tunashuka kwenda kuiteka.”

⁷⁰ Ni kama mtu mmoja akienda kule na kuiteka Urusi, majeshi makubwa kuliko yote ulimwenguni. Lakini alifanya hivyo kwa sababu alikuwa na kongamano na akalizungumzia na Kristo.

⁷¹ Hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo. Kanisa la Kipentekoste usiku wa leo, linahitaji kongamano, kuitwa pamoja, kuzungumza na Mungu kuzirudisha nguvu za Kipentekoste za mtindo wa kale, Roho Mtakatifu, kurudi kanisani, na kuihuisha imani, na kufanya mikutano iliyokuwako.

⁷² Lilikuwa ni kongamano kwelikweli. Lakini basi wakati Yeye... Kuna aina nyingine ya kongamano. Baada ya mtu kufuata agizo la Mungu, kama Musa alivyofanya, na kuwatoa wana wa Israeli kutoka Misri, naye alikuwa akienda zake kwenye nchi ya ahadi, moja kwa moja katika njia ambayo Mungu alimwambia aende, ndipo basi akakabiliwa na kizuizi.

⁷³ Hivyo ndivyo kanisa limefanya usiku wa leo, hivyo ndivyo wengi wetu tumefanya maishani mwe—mwetu, tunakabiliwa na jambo fulani, lakini kama ni la kuzuia ahadi, kama kitu chochote kinaizuia ahadi, tuna haki ya kufanya kongamano.

⁷⁴ Hawa hapa Israeli, Musa akiwaongoza, ile Nguzo ya Moto ikiwatangulia, na hii hapa Bahari ya Shamu ikiwakatilia mbali kutoka Palestina. Moja kwa moja kwenye mstari wa baraka, hii hapa Bahari ya Shamu inakuja, na jeshi la Farao nyuma yao, na milima pande zote mbili. Hata maumbile yangepiga mayowe yapate rehema.

⁷⁵ “Loo,” Israeli wakasema, “ingalikuwa heri kwa Mungu kwamba tungalikufa huko chini pamoja na sufuria za nyama za Misri! Afadhali tungalifia kule chini, kuliko kuja huku nje na kuuawa na Farao.”

⁷⁶ Lakini Musa, yule kiongozi mkuu wake, alifanya kongamano na Mungu hapo awali, alijua maana ya kuwa katika mahali pagumu.

⁷⁷ Watu wengi ambao wamezaliwa nusu, waliozaliwa nusu njiani, wajukuu... Kama David du Plessis alivyosema hivi majuzi usiku, “Mungu hana wajukuu, Yeye ana wana na binti pekee.” Lakini inapofikia mahali ambapo mjukuu, ambaye ndio kwanza aingizwe na, ati kwa maana mama yake alikuwa Mpentekoste, ama baba yake alikuwa Mpentekoste, anakuwa sehemu ya kanisa, la, bwana, hana budi kuzaliwa kama tu baba yake alivyojaliwa, maana Mungu hana wajukuu. Hana budi

kupata tukio. Hawezi kuingia kwa tukio la baba, ama tukio la mama, huna budi kupata tukio lako mwenyewe. Huko kulikuwa kuzaliwa kwao, mwajua, huna budi kuzaliwa, pia.

⁷⁸ Mungu hawatambui wajukuu, hana wowote; wote ni wana na binti.

⁷⁹ Unasema, “Vema, nilizaliwa, na mama yangu na baba yangu walikuwa Methodist, nami nilipelekwa katika kanisa la Kimethodisti.”

⁸⁰ Hiyo ni sawa, bali wewe ni mjukuu mpaka utakapozaliwa kwa Roho wa Mungu, ndipo wewe si mjukuu.

⁸¹ Sasa, Mungu alikumbuka ahadi Yake, Naye alikuwa amementuma Musa. Nao walikuwa wamewaongoza hao watoto hadi mahali hapa, na moja kwa moja kwenye wajibu, wa kuwaongoza wana wa Israeli, kizuizi kikaingia njiani.

⁸² Ninyi, mlio nje usiku wa leo, wengi wenu ni wagonjwa. Labda ninyi ni watumishi halisi wa Kristo, na mmefanya yaliyo mema, kadiri mjuavyo, lakini kansa ilipitia njiani mwako, uvimbe, upofu, ukiziwi, kilema, kitu fulani kilipitia njiani mwako kwenye wajibu, basi ni wakati wa kuitisha kongamano, ni wakati wa kufanya jambo fulani kulihusu.

⁸³ Musa anaenda nyuma ya mwamba, naye alikaa huko mpaka alipopewa amri za kusonga mbele.

“Utafanya nini, kumrudia Farao?”

⁸⁴ Akasema, “Waambie wana wa Israeli, kwamba wasonge mbele.” Hilo...Jeshi la Mungu—la Mungu daima husonga mbele, hakuna kurudi nyuma hata kidogo, hakuna kurudi nyuma katika jeshi la Mungu, Yeye hana hayo, tunasonga mbele.

⁸⁵ Ndipo akatembea hadi kwenye Bahari ya Shamu, na alipofanya hivyo, akainua fimbo ya Mungu mbele ya Bahari ya Shamu, nayo ikafunguka nao wakavuka juu ya nchi kavu. Mungu hufanya njia ya kuepukia. “Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu anapenda kuwaokoa kutoka kwa hayo yote. Na wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu watakata mateso.” Kongamano lilifanywa, amri zikatolewa, nao wakasonga mbele.

⁸⁶ Kulikuwa na kongamano lingine. Tungeweza kutaja mengi, lakini maskini hao watu wanaosimama huko nje wanatetemeka. Sikilizeni, kulikuwako na kongamano lingine lililofanywa, ambalo lilikuwa huko Gethsemane, usiku mmoja. Wakati Kristo alipokuwa amempendeza Mungu, mpaka akaagiza kongamano, na kusema kitu kama hiki: “Hivi unataka kupitia hayo, ama utarudi nyuma?”

⁸⁷ Ndipo uamuzi ukafanywa: “Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke.” Ni kongamano la jinsi gani! “Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke.”

⁸⁸ Kulikuwa na kongamano lililofanywa, pia, pale Kalvari. Kulikuwa na kongamano lililofanywa katika ukumbi wa hukumu wa Pilato, “Ni nani atakayesimama huku mgongo wake umeelekezwa kwa mjeledi?” Kwa kuwa nabii alisema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Kongamano liliagizwa, naye Yesu akachukua mahali hapo, maana Yeye alikuwa Ndiye pekee ambaye angeweza kupachukua mahali hapo, hakuna mtu mwingine angaliweza kufanya hivyo. Naye alipachukua, kwa sababu alitupenda.

⁸⁹ Yeye yuko tayari kulizungumzia lote pamoja nasi usiku wa leo, kwa ajili ya chochote alichotesekea pale, kwa kuwa alipachukua mahali petu. “Adhabu yetu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*,” wakati uliopita. Atalizungumzia pamoja nasi.

⁹⁰ Halafu, ninataka kuzungumza kwa ufupi juu ya kongamano lingine, kulikuwa na kongamano lingine lililofanywa. “Kanisa jipya linapaswa kuwa Kanisa la aina gani, Kanisa la Kikristo? Je, tuliendeshe kwa *nanii*, ama yatupasa...? Tunapaswa kulifanya namna gani? Linapaswa kuwa Kanisa la aina gani? Linapaswa kuwa ni dhehebu, ama litakuwa ni ushirika, ama litakuwa *hivi*, *vile*, ama *vinginevyo*, au watakuwa tu kitu fulani kilichochaguliwa?” Kwa hiyo kulikuwa na kongamano lililofanywa Mbinguni. Daima kunapokuwa na kongamano, ulimwengu mzima huketi na kungojea.

⁹¹ Hapa wakati fulani uliopita, mhudumu mmoja aliniambia, alisema wakati Mussolini alipokuwa akifanya ninii yake, akifanya kongamano hili wakati wa vita vya pili vya dunia wakati ulimwengu wote, kila mtu, alihusika (Baadhi ya watu wakizozana kwa sababu hawakuwa na sukari kwenye kahawa yao, sukari ya kutosha, huku watu wakifa kondeni; sisi ni watu wasio na shukrani.), naye akasema alikuwa anatembea sakafuni, hakujua la kufanya, akiangalia na kusikiliza matangazo haya ambayo Mussolini alikuwa akitangaza, jinsi atakavyovamia na kadhalika, mambo ambayo alikuwa akizungumzia.

⁹² Ndipo akasema mtu fulani alibisha mlangoni, basi yeye akaenda mlangoni, na kusema mhuni mamboleo, amesimama pale huku nywele zikining’inia shingoni mwake, na masharubu usoni mwake, na kusema, “Nataka uende katikati ya mji, unisaidie kuuza mashairi yangu. Hakuna mtu anayetaka kulizungumzia.”

⁹³ Kasema, “Ingia ndani mtu wangu, na uketi chini kwa dakika moja. Ninavutiwa sana hapa, kuna kongamano linaloendelea, nami ninangojea kusikia matokeo yake, yatakavyokuwa, kwa sababu yana—yanamaanisha mengi kwa taifa letu na maskini wavulana wetu ambao itawabidi kufia uwanjani.”

Kasema, “Nina hamu ya kusikia matokeo ya kongamano hili yatakavyokuwa.”

⁹⁴ Huyo mhuni akaruka kati yake na redio, na akaendelea kusema, “Lakini ma—ma—mashairi yangu ni muhimu zaidi.” Loo, jamani! Alimshika tu mkono, akamwongoza hadi mlangoni.

⁹⁵ Tunapongojea kongamano! Usiku wa leo, tunapaswa kungojea kongamano: Mungu kuamua kile kitakachotukia Tifton, usiku wa leo. Ni nani atakayeamini taarifa hiyo? Ni kitu gani kitakachotukia katika siku mbili ama tatu zijazo huku Tifton?

⁹⁶ Wakati watu hawa walipokwenda kwenye chumba cha juu, mia na ishirini, pamoja na Mariamu, na Simoni Petro, na wengine wao wakapanda kwenye chumba cha juu, ngazi ndogo inayoelekea nje ya hekalu, wakaingia kwenye chumba cha kale cha kuhifadhia ambamo taa ndogo za grisi zilikuwa zinawaka, kwa kuwa walikuwa wameamriwa na Bwana Yesu, “Ngojeni katika mji wa Yerusalemu, hata mtakapovikwa umezo utokao Juu. Ninapanda kwenda Utukufuni, nasi tutafanya kongamano, nami nitawaambia basi, jinsi Kanisa linavyopaswa kuendeshwa.”

⁹⁷ Walipokuwa wamekusanyika mahali pamoja na kwa nia moja, wakishangaa ni agizo la namna gani watakalokuwa nalo kwenda na kuagiza ulimwengu wote kwamba watu wote hawana budi kuwa na Kanisa hili la Kikristo, na ushirika ambao lingeanzisha, wakati walipokuwa wamekusanyika mahali padogo si pakubwa kuliko hapa, yapata watu mia moja na ishirini, mara ikaja sauti kutoka Mbinguni kama upopo wenye nguvu ukienda kasi, nayo ikajaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Kongamano lilikuwa limefanywa, uamuzi ulikuwa umetolewa.

⁹⁸ Ndugu, dada, usinielewe vibaya, hiyo ndiyo—ndiyo njia hasa ambayo kanisa la Kikristo linapaswa kuongozwa, kama ni kanisa la Kikristo. Kongamano la Mungu liliamua, ndipo Roho Mtakatifu akaja kwenye Siku ya Pentekoste, na kwa hiyo akawayumbisha watu hao kwa nguvu za Mungu, hata wakayumbayumba kama wanaume na wanawake walevi. Hayo ndiyo matokeo ya hilo kongamano.

⁹⁹ Baada ya kujazwa na nguvu nyingi na furaha nyingi, Petro akisimama katikati yao alisema, “Hawa hawajalewa kama mnavyodhani, kwa kuwa ni saa tatu ya mchana, lakini,” yeye akasema, “hili ni la Kimaandiko, *Hili ni Lile* lililonenwa na nabii Yoeli.” Mara nyingi nimetoa tamshi hili: Kama *Hili* si *Lile*, nitaliweka tu *Hili* mpaka *Lile* litakapokuja. “*Hili ni Lile* lililonenwa na nabii Yoeli; na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu: wana wenu na binti zenu watatabiri; juu ya watumishi Wangu na wajakazi Wangu, nitaimwaga Roho Yangu; nami nitaonyesha

ishara katika mbingu juu, na katika nchi chini, nguzo za moshi na mvuke.”

¹⁰⁰ Naam, kulikuwa na kongamano lililofanywa. Na halafu siku chache, yapata siku kumi baadaye, walikuwa wameanza kupitia lango lililoitwa Zuri, watu wawili, Petro na Yohana, na hapo alilala mtu aliyekuwa kiwete, ama alikuwa kilema tangu tumboni mwa mamaye. Na hiyo inathibitisha ya kwamba walikuwa ni wahubiri wa Kipentekoste, walisema, “Fedha na dhahabu, sina, sina pesa zozote; lakini nilicho nacho. . .”

¹⁰¹ Hicho ndicho Wapentekoste wanachohitaji leo hii, kile walichokuwa nacho, hicho ndicho upungufu kanisani leo hii, si Pentekoste tu, bali Baptisti, na Presbiteri, na Methodisti, hicho ndicho kilichotupungukia sisi sote.

¹⁰² “Nilicho nacho, nakupa: Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama utembea,” wakamwinua kwa mikono, naye akapata nguvu na kuanza kurukaruka na kumsifu Mungu wakati akiingia hekaluni.

¹⁰³ Mafarisayo wakatoka, na kusema, “Hawawezi kufanya mkutano kama huo mjini, kwa sababu ungeleta tu matokeo mabaya.” Kwa hiyo, wakawaleta pamoja kwenye Mahakama ya Wazee, na kuwapiga bila huruma, na kuwaweka mbele ya baraza la wazee wa mahakama ya Wazee. Ndipo waliposimama mahakamani, nao wakasema, “Tunaona kwamba wao ni wasio na elimu wala maarifa,” hakuna seminari waliyopata kuwa na ujuzi wake, “lakini ilitubidi kuwatambua, kwamba walikuwa pamoja na Yesu,” kwa sababu mambo yale yale Yesu aliyofanya, walikuwa wanafanya. “Ilitubidi kutambua kwamba walikuwa pamoja na Yesu.”

¹⁰⁴ Loo, hilo ndilo kanisa linalohitaji siku hizi, nguvu kubwa sana hata itawabidi kutambua kwamba mumekuwa pamoja na Yesu. Hiyo ndiyo shauku ya moyo wangu, kuishi maisha ambayo watu wanajua ya kwamba Kristo anaishi ndani yetu.

¹⁰⁵ Loo, ni wakati wa jinsi gani! Ndipo walipoachiliwa, walipowapiga na kuwaambia wasihubiri tena katika Jina la Yesu, waliwatisha zaidi kisha wakawaacha waende, walipoachiliwa, walienda kwenye maskini kundi lao wenyewe. Walipokutana, watu walikuwa wakija kutoka sehemu zingine, wakisema, “Tuliteswa vivyo hivyo. Tufanye nini?” Kwa hiyo wakafanya kongamano. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Hilo ni jambo zuri, la busara. “Tumetishwa, na tumekuwa *hivi*, na tumepigwa, hebu tufanye kongamano.”

¹⁰⁶ Basi walipokusanyika pamoja, wote walipiga magoti katika kongamano hili, na kuomba kwa moyo mmoja, kasema, “Ewe Mungu, imeandikwa katika Maandiko, ‘Kwa nini makafiri wanafanya ghasia na watu kuwazia ubatili.’ Wape watumishi Wako ujasiri wote kunena, na nguvu za kuunyosha mkono wa

Mtoto Wako Mtakatifu, Yesu, kuonyesha ishara na maajabu na uponyaji.”

¹⁰⁷ Basi kongamano hilo lilipokwisha, maagizo yakaja, nayo yakalitikisa hilo jengo ambamo walikuwa wamekusanyika pamoja, nguvu za Roho Mtakatifu. Nao wakaenda wakihubiri Neno, kila mahali, kwa ujasiri, wakiunyosha mkono wa Yesu Kristo juu ya watu kwa imani na kuwaponya wagonjwa.

¹⁰⁸ Mungu anataka kulizungumzia pamoja nasi usiku wa leo. Kuna nini? Tumepoteza kitu fulani mahali fulani, kama mambo hayo bado hayaendelei. Anataka kufanya kongamano pamoja nasi, kulizungumzia. Sasa, nipo hapa kujiunga nanyi katika kongamano hili.

¹⁰⁹ Sasa kuna kongamano moja tu zaidi ambalo ningetaka kulizungumzia kabla tu ya kufunga, na hilo ni hili: Kongamano la Hukumu. Huenda hukuhudhuria UN, huenda hukuwa kwenye Shirikisho la Mataifa na makongamano yao, huenda hukuwa kwenye mkutano mkuu wa Assemblies of God, ama kongamano kuu la Church of God, ama kongamano kuu la Methodisti, ama—ama kongamano lolote lile, huenda hukuwa kwenye lile la Mabingwa Wanne, huenda hukuwa huko Geneva, lakini kuna jambo moja la hakika, utahudhuria hili la mwisho.

¹¹⁰ Sote tutakuwa huko, nasi tutatoa hesabu kwa kila kitu ambacho tumefanya. Na wakati Maandiko yanapokuja mbele zetu, “Dhambi zenu zikapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji. Njoni sasa, na tusemezane, asema Mungu.” Tutasema nini wakati huo?

¹¹¹ Loo, huenda mtu fulani akasema hivi, ningetaka kuwaambia watu hawa ndani na nje, huenda ukasema, “Lakini, Mhubiri, mimi ni mtu maskini tu, Mungu kweli hanihitaji.”

¹¹² Loo, naam Yeye anakuhitaji. Kuna mahali padogo katika moyo wa Mungu, unasema ule wimbo, wala si zaidi ya wimbo, hata hivyo, ni kweli, kwamba hakuna mtu mwingine anayeweza kupachukua mahali hapo ila wewe. Mungu anazungumza nawe, ni wewe, wewe ndiwe tu ungeweza kutimiza sehemu hiyo katika moyo wa Mungu, Anakungojea. Anataka kulizungumzia nawe. Anataka kufanya kongamano pamoja nanyi, “Njoni msemezane kabla haijawalazimu kukutana na Hukumu hii, kwa sababu itakuwa mbaya sana wakati huo.” Nawe huwezi kulizungumzia wakati huo, umechelewa sana wakati huo.

¹¹³ Unasema, “Lakini mimi ni ombaomba tu.”

¹¹⁴ Sijali wewe ni kitu gani.

¹¹⁵ “Mimi ni mlevi. Mimi ni mwa—mwa—mwanamke mzinifu. Nimefanya kosa mhubiri, ni—nimeishi bila uamninifu kwa nadhiri zangu za ndoa, ama—ama nime—nimefanya mambo ya utovu wa maadili. Nimekunywa pombe, nimevuta sigara, nimecheza kamari, nimeiba, nimedanganya.”

¹¹⁶ Sijali umefanya nini, Mungu alikuwa, kasema, “Njoo, tusemezane; huenda dhambi zako zikawa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji kama utakuja tu tulizungumzie kidogo. Tunakuhitaji.”

¹¹⁷ Wakati fulani uliopita, kulikuwako na ninii, mjini, vema, afadhali nisilitaje hilo jina, bali kulikuwako na maskini ombaomba ilivyoonekana, maskini msokwao mtaani, ambaye alikanyagwa na motokaa. Loo, mifupa yake ilivunjika, na mikono yake ikavunjika, na uso wake ukapondwa kabisa, na damu ikitoka, naye aligongwa akapoteza fahamu. Kwa hiyo mamlaka ziliita gari la kuchukulia wagonjwa, nao wakamkimbiza kwenye hospitali fulani kubwa.

¹¹⁸ Ndipo kengele ya dharura ikalia, nao madaktari, wakasema, “Ni dharura, hamna budi kukimbia kwenye wodi, upesi. Basi madaktari walipokusanyika, walimwona amelazwa pale juu ya ninii, amenyoshwa mezani, damu ikitiririka kutoka machoni mwake, puani, mdomoni, na masikioni mwake. Huyu mzee alionekana kupoteza fahamu. Wakamtikisa, nao wakamchunguza kidogo, na kusema, “Loo, jamani! Miguu yake imevunjika, mikono yake imevunjika, mbavu zake zimevunjika.” Wakasema, “Hebu na tufanye kongamano kidogo, tuzungumzie hili.”

¹¹⁹ Wakati wa lile kongamano, yule mzee akarudia fahamu zake, nao madaktari, wakifanya kongamano lao, wakasema, “Yeye si kitu ila ombaomba, haina faida kutumia muda wetu kujipumbaza naye.” Ndipo waliporudi, kasema, “Mfungeni tu.”

¹²⁰ Yule jamaa mzee akageuka, akasema, “Nina thamani fulani,” alisema, “Mungu alinipenda sana hata akamtoa Mwanawe wa pekee ili nipate Uzima wa Milele, na, hakika, ninastahili dakika chache za muda wenu. Nimehubiri Injili mitaani, na kila mahali, kwa miaka hamsini.” Kasema, “Nina thamani ya kutosha kwenu kuishughulikia miguu yangu, na kuiunganisha tena, ama chochote kile.” Kasema, “Mungu alinipenda, Naye akamtoa Mwanawe kwa ajili yangu, nami nina thamani fulani.”

¹²¹ Hakika, una nafsi ambayo ina thamani ya ulimwengu elfu kumi. Lizungumzie pamoja Naye usiku wa leo, rafiki, maneno machache tu yatamaanisha mengi sana. Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu sasa. Ningetaka kila mmoja wenu awazie moyoni mwake, “Je, nina thamani yoyote?” Hakika, unayo. Mungu anakupenda, angalia kile alichotoa kwa ajili yako.

¹²² Vema, ninajuaje Yeye atakupokea? Wazo lenyewe la wewe kutambua kwamba umekosea, ni ukweli kwamba Kristo anashughulika na wewe. Yeye alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Hiyo inaonyesha ya kwamba Mungu yuko papo hapo karibu nawe, akikuvuta. Anataka kufanya kongamano dogo pamoja nawe,

hapo kitini mwako, ama ukisimama kwenye marefu ya kanisa, ukutani, ama nje, ukiegemea kwenye hili jengo, ama huko nje kwenye magari yenu, Roho Mtakatifu. Loo, najua inaonekana rahisi. “Nimesikia hayo hapo awali, wewe. . .” Lakini ni kweli. Anataka kufanya kongamano dogo pamoja nawe sasa na kulizungumza pamoja nawe.

¹²³ Labda baadhi yenu ni wagonjwa na—nanyi—nanyi mnataka Mungu awaponye, nawe ungesema, “Ee Mungu, nina shida gani?” Mungu anataka kulizungumza pamoja nawe. Sasa chunguza moyo wako uone kuna shida gani.

¹²⁴ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, sijui ni wangapi ambao ningeweza kuona. . . Si lazima uone, Mungu anaona. Kama uko kwenye gari lako, nje au ndani ya jengo, naomba tu kwa utulivu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa na macho yenu yamefumbwa, inueni tu mikono yenu, na useme, “Mungu, ningetaka kuzungumza Nawe, usiku wa leo.” Mungu awabariki. Loo! “Ningependa. . .” Loo, huko nje kila mahali, popote ulipo, “Ningependa tu kulizungumzia, Bwana.” Mungu awabariki.

¹²⁵ Mikono ishirini ama thelathini imeinuliwa humu jengoni. Sioni, siwezi kuona kupitia gizani huko nje, ama katika magari, bali Mungu anamjua kila mmoja wenu. Mngetaka kulizungumzia, vema, hebu tuagize kongamano sasa hivi, kwa kuwa Yesu alisema, “Kama kuna wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa miongoni mwao.” Na hapa kuna karibu thelathini ndani. “Nitakuwa miongoni mwao, na—na tutalizungumzia tu.”

¹²⁶ Hakuna nafasi ya kutosha kwa ajili ya wito wa madhabahuni, kuja madhabahuni, bali popote ambapo Mungu amesema nawe, hapo ndipo, anapozungumza nawe, hapo ndipo anapotaka kungea nawe, moja kwa moja katika dhambi zako ama katika kutokuamini kwako, ambako ni dhambi.

¹²⁷ Kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Unasema uongo, unaiba, unakunywa pombe, kwa sababu huamini; kama ungekuwa ni mwaminio, usingefanya hivyo. Kwa hiyo kuna dhambi moja tu, na hiyo ni kutokuamini. Labda wewe ni mfuasi wa kanisa ambalo haliamini Biblia nzima, hiyo ingali ni dhambi. “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa,” alisema Bwana wetu.

¹²⁸ Hebu na tulizungumzie pamoja Naye sasa. Na tuinamishe, tuendelee kuinamisha vichwa vyetu, nawe uombe papo hapo ulipo, useme, “Bwana, nimefanya *hivi-na-hivi* na *hivi-na-vile*, lakini Wewe uliniahidi.”

¹²⁹ Atasema kama alivyomwambia Musa, “Ninakumbuka ahadi Yangu, nami nitashuka kuja kukukomboa.”

¹³⁰ Kama ni maradhi, sema, “Bwana, huenda nimekosea. Kama mahali popote, loo naam, ninakumbuka jambo

fulani nililofanya, Bwana, nitaenda nisahihishe hilo.” Hebu tuzungumze Naye, ndipo kwa kupigwa Kwake umeponywa.

¹³¹ Sasa, Baba wa Mbinguni, kwa kuwa miguu inauma na nyayo kuumia, miili imepozwa na hewa baridi sana, nami nimezungumza kirefu, lakini ninawazia, Bwana, juu ya huzuni hiyo ya moyoni na hiyo Yordani baridi ya kuvukwa moja ya siku hizi, tutakapofikia mwisho wa safari ya maisha, basi itakuwa ni wakati wa kutisha sana.

¹³² Ninawazia juu ya wagonjwa, ambao labda wamesimama karibu wakiwa na ugonjwa wa moyo, na wakiwa na kifua kikuu, na mateso mengine mengi, labda kansa, na, loo, wao ni wagonjwa na wahitaji, nao wameketi wakisikiliza, bali wana kongamano dogo pamoja Nawe sasa.

¹³³ Huenda kuna wale ambao hawajawahi kukukubali Wewe, nao wametenda dhambi, na wamefanya mabaya, nao wamekosa kuiamini Injili, na, ama labda wameenda kanisani na kufanya maungamo ya hadharani, lakini bado hawajazaliwa kwa Roho, kwa sababu kwamba walidhani, “Vema, lilikuwa ni neno la kilokole kwa Kristo.”

¹³⁴ Mungu, ninaomba ya kwamba utazungumza nao, useme na mioyo yao, chochote wanachohitaji. Waliinua mikono yao, Nawe ulisema katika Neno Lako Mwenyewe ya kwamba, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Halafu tena ukasema, “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu. Nami nitawafufua katika siku za mwisho.” Uliliahidi, Bwana.

¹³⁵ Yohana Mtakatifu 5:24, Wewe ulisema, “Yeye alisikiaye Neno Langu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni kamwe, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Hizo ni ahadi Zako, Bwana.

¹³⁶ Imeandikwa katika Maandiko ya kwamba, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Bwana, kumbuka ahadi Zako usiku wa leo, tunapofanya kongamano hili dogo.

¹³⁷ Jalia nguvu za Roho Mtakatifu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini, jalia zije juu ya kila mtu anayeona njaa na kiu usiku wa leo. Na jalia mazungumzo haya madogo yatoshe, Bwana, kuwafufua wapate afya mpya. Wape vipofu kuona, wa kimwili na wa kiroho pia, ipe afya miili minyonge, dhaifu, inayotetemeka, Ee Roho Mtakatifu, zipe amani na faraja nafsi zinazoteseke, na msamaha wa dhambi kwa wale waliotoka njiani.

¹³⁸ Tujalie, Baba, na Jina Lako litasifiwa kwa ajili yake, kwa kuwa sasa tunaweza kuwaleta Kwako, nao waliomba. Na sasa tunawakabidhi Kwako kama kumbukumbu za ibada, na za Ujumbe. Tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwanao.

¹³⁹ Huku tumeinamisha vichwa vyetu sasa, litafakarini, zungumzeni Naye kidogo tu, ndani na nje. “Bwana nimetenda dhambi, nimefanya makosa, nami nina thamani fulani. Nina thamani kubwa sana hata ukamtuma Yesu, Naye akafa ili niweze kuokolewa, na ni—niweze kuponywa, na kwamba ningekuwa na, afya njema, Nawe ulisema katika Biblia Yako, ‘Ni—ningetaka zaidi ya mambo yote mfanikiwe katika afya.’ Nina haki kwake, Baba, nami ninataka kuzungumza Nawe sasa hivi,” ndani na nje.

¹⁴⁰ Basi mwombeni awafanyie mambo haya, nami nina hakika atayafanya. Yeye yupo hapa sasa kukufanya mzima, na kukuokoa na dhambi zako, na kuondolea mbali uovu wako wote, na kufuta makosa yako yote, na kuyaponya maradhi yako yote na magonjwa, na kukufanya mzima, mwache tu Yeye afanye hivyo.

¹⁴¹ Huku tumeinamisha vichwa vyetu, na tunamngojea Yeye kutimiza kila ahadi huku mkisimama kwenye kichaka kinachowaka moto sasa, ningependa kanisa, ninyi mnaoendelea kuinamisha vichwa vyenu, ndani na nje, basi hebu tuimbe wimbo. Mwajua, katika Maandiko waliimba wimbo, ndi—ndipo Roho wa Mungu akaja juu ya watu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴² Hebu, ninajua, huu hapa mmoja tunaoujua sote: “Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza.” Tuna hakika ya kwamba mnaujua wimbo huo. Hebu tuimbe pamoja kwa utulivu sasa. Labda tunaweza kuuimba bila muziki, dada.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza (Loo!)
...kunua wokovu wangu
Juu...

Hiyo ni kwa ajili ya uponyaji, ama dhambi, wokovu wangu.

Nampenda,

Wazieni tu wema Wake.

Kwani Yeye kwanza...
Na kunua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁴³ [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.] Huku mmezungukwa na utamu huu, nanyi mnaendelea kuimba: Mnaamini Uwepo Wake u pamoja nanyi? Kama mnaamini, inueni mikono yenu, na kusema, “Tangu usiku huu na kuendelea, ninajitolea mwenyewe upya sasa. Ninakubali uponyaji wangu, ninakubali ombi langu la wokovu,” ndani na nje. “Ninaamini ya kwamba Kristo, Mwana wa Mungu, sasa atashughulikia yote ninayohitaji. Mnaweza kuinua mikono yenu? Huku tukiimba kwa utulivu tena, huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

Na...

¹⁴⁴ “Kila haja niliyo nayo, ninaamini ya kwamba Yeye ataitimiza, wakati kongamano hili linapoendelea.” Nje, ndani ya gari, kama wewe ni mgonjwa, umelemaa, simama.

...penda...

¹⁴⁵ Kama wewe ni kipofu, geuza kichwa chako kuelekea Mbinguni, na uitazame Nuru; kama wewe ni kiziwi katika sikio moja, weka kidole chako katika sikio lako zima.

...wokovu

Mtini Kalvari.

¹⁴⁶ Loo, utamu huo uliobarikiwa! Ukikaribia kile kichaka sasa, hisi matokeo ya Moto kichakani, Roho Mtakatifu akizipasha moto nafsi zetu kwa imani.

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

Na-...

¹⁴⁷ Kama kuna dhambi maishani mwako, ikiri kama dhambi, mwambie Mungu unaisikitikia, Yeye atakuchukua sasa hivi.

Kwani...

¹⁴⁸ Je, unaweza kuhisi Uwepo wa ninii Yake... wa kile kichaka, huku umepiga magoti hapo kwa imani, Uweponi Mwake?

Na kununua wokovu wangu... 

60-0108 Kongamano Pamoja Na Mungu
Unity Tabernacle
Tifton, Georgia Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org